Interjection: But of course you know people are talking about redistributing the land back to them. How do you manage interest of the indiginous people in terms of getting the lands and the national interest?

Mheshimiwa (Hon. Mutiso): I will answer that may be, I don't know who are talking to myself, I have property there and a place actually where people park settles there, that's what I'd call, newly settled areas. Because of the pressure of land as I told you, people went down looking for land and pasture. And what happened is that is between 1969 say 70 that is when we had the first (not clear). That was a trust land and it was named like a game reserve. So after people settled there, they somehow were living in the game reserves, not the national parks. That is Kyulu ranges hapo so later on, the government recognised that habitation. Okay? After it recognised that habitation if conferred some loose rights to those people, to live harmoniously with the game. So long as there's no interference of the game because this interest of that time was at least to these people somewhere.

Now, after they settled there, the provincial administration was set there to help the people at least to survive or to live. Now later on what happened is, the government de-gazetted part of the game reserve and gave to these people but in 1990-91 there, the truth let it be said, when they had the emergence of the opposition, because I remember even the president himself decree

event those people be given title deed. Then because of the emergence of the opposition. I remember even time one of our leaders went there, he was heckled, he was abused and he was told, you are not taking care of our interest, and as such, they were left alone.

Those title deeds, they had processed them but they were stopped. But we went there last month and I can assure you that problem is going to be sorted out what I would suggest, there's a genuine concern. The revenue which is coming from the adjoining regions, for example new here, obviously we have a factory built here may be for processing fruits or plants or whatever the case may be, we expect the County Council to benefit and the same way we also expect the County Council to provide the basic amenities. Just the same way, what we are saying is as much as you would like to say that land is this and that and that the point is can we have a small fraction of the revenue coming to that passed to these people, just like in Maasai Mara, Narok, they are paying something out of the gate collection, they give 5% to the local Community just as a good gesture because this country is ours. So where is the money going after all. It is our money. But that money is collected there, and I am maybe X, Y and Z, I am the minister and when I go to treasury, because I have been blessed by God to be a minister, maybe by design or whatever have the privilege of dipping my hand in the government coffers and taking the money as I want.

So, what we are saying is, at least as we have other people putting their hands in the public coffers, let us also have the local people having the right to also put their hands to the public coffers. That's all I can say Okay. Are you satisfied? Thank you.

Thank you very much Honourable Mheshimiwa for that long suffitionsThomas Kimeu?

Thomas: Kwa majina naitwa Thomas Kimeu, mimi niko na machache ya kusema. Na kwanza ni kuhusu rais: Rais akuwe chini ya sheria. Fikira ya kwanza.

Com. Kabira: Endelea

Thomas : Ya pili, Bunge ikiichaguliwa, bunge ikifungwa, speaker awe anashikilia hiyo waadhifa. Tatu : Wakati bunge imevunjwa kila mtu anayegombea hii kiti ya rais awe anatumia mali yake, kama ni magari ya serikali, irudishwe afanye uchaguzi na gari yake. Ya nne kama unagombea hii kiti ya Urais na ulikuwa rais, hii jina ya rais iwache kutajwa. Iwe inasemekana mtu fulani anapiga campaign mahali fulani. Sababu saa hivo sio rais. Ya tano: Mawaziri wachaguliwe na bunge. Nataka kufika hapo.

Com. Kabira: Wacha tupatie Pastor Job Wafula.

Job: Asante kwa nafasi hii kama mlivyosikia jina yangu ni Job Wafula naka Sultan katika kiu location. Hapa kasikeu

division. Ninayo machache ambayo ninayoangalia kama ikiweza kutusaidia katika sheria zetu nchini. Labda ninaongea katika kiswahili maana unaandika kidogo, ningeonelea kama maoni yangu yenyewe labda mengine yameshawahi kuzungumziwa lakini katika maoni pia yangu, naonelea President au Rais wa Kenya, mamlaka ile aliyonayo ni makubwa ipunguzwe kwa kiasi kwamba kuna sehemu zingine ambazo yeye anachukuwa au yeye anafanya ambazo wananchi wanaumia pia. Kama vile wamesungumzia kama vile, kuchagua chief justice, si hangekuwa ni yeye ambaye maana akichagua anamamlaka juu yake. Tunaoelea ya kwamba chief justice, ofisi hiyo iweze kutangazwa halafu watu wawezi kutuma maombi yao. Na katika hao either wawili wawezi kuangaliwa kati yao ambao wanaweza kufanya kazi hiyo. Na akiwa amechaguliwa na president, wakati wowote atafanya lolote lile ambalo lina favcur president na sio katika kazi yake kwa hivyo ningependa president asichague chief justice, katika hiyo ofisi jambo la pili pia, katika hali hii ya makampuni au zile sectors ambazo zinazotumia pesa nyingi, utakuta ya kwamba katika sehemu nyingi, pesa zimeibiwa na watu ambao wamewekwa hapo kama wakurugenze. Halafu baada ya muda utakuta kwamba watu ndio wanatambulikana kwamba wamekula hizo pesa. Lakini hakuna njia ya kurudisha hizo pesa, turudi mahali pale, tufanye kazi ile ambayo ilikuwa imedhaminimwa kufanywa. Kwa hivyo, kama mtu akipatikana ya kwamba ameiba katika sehemu fulani au amenyakuwa kwa mfano kama mbunge wetu alikuwa akasema, akiona mahali ambapo kuna pesa kidogo na anataka kuwafikia wananch, akichukuwa hizo pesa na zisifanye hiyo kazi ambayo zilikusudiwa kufanya, huyo mtu afuatwe arudishe pesa hizo ziende zifanye kazi hiyo kwa sababu watu wanaumia katika sehemu ingine na wengine wanakula. Jambo lingine ni kwamba kimezungumziwa kwa upana, kuhusu sheria ya ardhi. Ardhi kama vile tumeona kwamba sheria hizi nyingi zimebuniwa katika wale wakoloni waliketa katika nchi hii yetu.

Ningeonelea ya kwamba hii title deed, ambayo inachukuwa nafasi kubwa kwa mwananch ambaye hata subuka kupata hiyo title deed, ni ngumu haingekuwa na mamlaka kwa mwananchi kutumia hiyo title deed kukopa loan ama kufanya nini. Ingekuwa na kikao fulani ambao inaweza kukaa na kuona ya kwamba huyu mtu anahitaji loan na apendekezwe au awe na wadhamini wale ambao wanaweza kusimamia na apate loan bila hiyo title deed kukopa. Kwa sababu inaumiza watu wengine na wengine hawaumii jambo lingine ni kwa kwamba katika upande wa mashamba tu, unakuta kwamba amechukuwa ma acre kama maelfu na ile hali mwingine hana hata mahali pa kuweka nyumba peke yake. Mimi nigeonelea kwamba sheria ingebuniwa ya kwamba kila mtu awe na kiasi fulani ya mashamba ile kwamba. Kama kuna mtu ambaye anashamba kubwa, agawie wengine maanake si sote ni raiya wa Kenya, ili kwamba hivo ambaye ana acre kubwa agawie wale watu ambao wanaitwa maskowtas. Maskwotas hawa wanatoka wapi na ni riaya wa Kenya wanafaa kuwa na nchi yao, wanafaa kuwa na mahali pa kulima.

Kwa wale watu ambao wamechukuwa hata kama wamenunua na pesa zao hizo pesa ambazo zinaitwa zao hao ndio wanao filisha serikali, kuiba katika kampuni halafu wanakuja wanasema ni pesa zao. Kila mtu aweze kuangaliwa hata kama amenunua shamba, hiyo shamba amenunua na pesa za wananchi ambao amewaibia halafu anakuja kunyanyasa tena kuwanyang'anya shamba lao. Kwa hivyo ningeonelea kwamba, mashamba yawe na kiwango fulani kwa kila mtu ambaye anachukuwa shamba. Na la sivyo hawa watu waangaliwe na waondolewe, ili wape nafasi wengine. Pia katika hali hiyo tu ya masomo, unaona kila wakati tunaambiwa ya kwamba, masomo ni ya bure. Lakini pamoja na hayo wale ambao wanaimba uko ya kwamba ingawa masomo niya bure huku chini, masomo si ya bure. Watu wananyanyaswa. Mtoto akiwa hana pesa hawezi kuenda shule lakini

katika wimbo wetu tunaimba kwamba primary school education is just free. Lakini, ukiangalia kutokea katika grassroot mtakuta ya kwamba it is not free, maana wazazi wanaumia. Pesa hata kama ni ndogo ndogo, lakini maisha wakati huu imekuwa ni ngumu sasa watoto hawasomi bure. Inafaa waangalie hiyo maneno kwamba. Kama ni masomo bure, wa provide kila kitu ambacho mtoto anafaa kutumia shuleni kama vitabu vya kuandika, vitabu vya kusoma. Serikali itoe au ipeane kwa hawa watoto. Maana kama hapo awali kulikuwa ni kwamba watoto walikuwa wanapewa vitabu. Kama sisi tukikuwa tunapewa hivyo kitabu exercise na whatever. Lakini kwa sasa hiyo vitu havipo na hiyo pesa ambayo zilikuwa zinatumiwa katika hiyo zilienda wapi? Huyu ndio nigeweza kuonelea kwamba, hayo kama wanataka ku-implement wacha ifanye kazi kama ni bure, hiyo vitu pia ipewe bure. Wabunge

Twenty five percent pia katika every province kumchagua President. Na isiwe kwamba miaka fulani ndio inapaswa President, President ni mtu ile ambaye watu wa nje wanaweza kuona ya kwamba ni President anaweza kutuongoza yeye achaguliwe bila kuangalia miaka ni mingapi bora awe ni mtu mzima ambaye anaweza kuamua mambo. Sio kwamba ni vijana ndio wanaweza kuongoza na wazee waende nyumbani, mzee, mzee anaweza kuwa mzee lakini ana hikima ya kuongoza nchi wacha aongoze maana uongozi unatoka kwa Mungu.

Naye makamu wa rais mimi ninge, ninge, ningeonelea ya kwamba makamu wa rais asichaguliwe na President tena. Maana wakati ma president anapomchaguwa makamu wa rais, mara nyingi hakuna kitu kile ambacho atafanya pasipo kumconsult president au kufanya kama vile anavoonelea. Makamu wa rais angechaguliwa na wabunge, wale ambao sasa baada ya president kuchanguliwa sasa katika bunge wachaguwe makamu wa rais hapo, maana president anachaguliwa na wananch naye makamu wa rais achaguliwe na bunge ile ambayo iko imechaguliwa kuingia kwa bunge. Iyo itaweza kurahisishia mambo ya kuzungumza kama kucorrect kama kuna mahali ambapo pa kusahisha asahishe, kwa ujasiri kwasababu hana mtu yule ambaye labda anaweza kusema ya kwamba atamuogopa lakini ana anasahihisha kazi hiyo na tutaweza kuendelea vizuri. Pia, katika hali hii ingine, eeh, wamezungumzia pia lakini nitaguza; mtu ambaye anayefanya kazi ya serikali astahili kuwa tena na business yake yoyote ile kwasababu akiwa nafanya hivyo mara nyingi kwa mfano kama madaktari, daktari ana anafanya kazi kwa serikali na pia ana nini pia Private clinic. Madawa yale ambayo yanapelekwa katika hiyo Private clinic inatoka kwa serikali. Hata ingawa wanaweza kubadilisha vibandiko ya kwamba ikikuwa ya G.K. lakini wanabadilisha kwasababu wakati huu ufiada umezidi na unaona ya kwamba mahospitali ya serikali haina dawa na inahali eeh, watu wale ambao mabinafsi madaktari wana madawa. Hayo madawa wanayapata kwa njia gani? Kwasababu wanataka kujinufaisha kwa njia isiyofaa kwahivyo ningeonelea ya kwamba kama ni daktari yule wa binafsi yeye angaliwe na akaguliwe yakwamba anatowa wapi madawa na hiyo mwananchi wa kawaida ataweza ku kuendelea. Pia cost sharing kwa upande mwingine inaumiza wananchi wale ambao labda hawana mahali pa kupata pesa. Kiasi kwamba akienda hospitali hata kama ni shilingi ishirini peke yake, huyo mtu hapati shilingi ishirini za kuenda kupata hiyo kadi. Ningeonelea ya kwamba hiyo katika ushuru ule ambao wana wanapata kwa serikali kama sasa kwa mfano kama budget inavyosomwa unakuta yakwamba kwa upande wa medical, au upande wa hospitali wamepeleka pesa fulani. Ingefaa kukadhiriwa pesa zile ambazo zinazo weza kutosha ku kumfikia mwananchi wa kawaida kama akiwa ingonjwa. Ndio unakuta people being unakuta wale ambao ni masikini wanakufa ovyo ovyo hata ugonjwa wa malaria kidogo tu kununua

madawa hiyo inamshida. Na sasa kama serikali ingeweza kuingia kwa jambo hilo kusaidia mwananchi wa kawaida bila shaka mwananchi wa kawaida angeweza kufanikiwa kupitia kwa mambo kama hayo. Kwa hivyo na hayo mengine ambayo sitaweza ku kuyataja maana tayari yamesomwa ningemba yakwamba nifikie mahali pale na Mungu wa uziwa awabariki.

Com. Kabira: Thank you very much pastor, aaah before I come to the councillor let me give Mr. Benard Mutinda a chance.

Benard Mutinda: Kwa majina ni hayo munasikia, Benard Mutinda na mimi na anzia na uchaguzi wa bunge. Tunaonelea kwa maoni yangu kama tunachagua wabunge wawe wakichaguliwa pamoja na councillors lakini uchaguzi wa rais uwe tofauti uwe peke yake. Kama rais tunachagua rais pale alikuwa amesimama kama chama vitatu ama vinne, ule anashinda na wapili warudishwe tena, wagombe wawili tuone ni nani atapita na percentage kubwa.

Eeh ya tatu rais anatakiwa ile mamlaka amepewa inarudhishwa chini kidogo kwa sababu unaona anasema leo huyu ndio vice president na akionelea anaanza kukaa kando kidogo, na vile yale yake anataka anamuambia hapana, wewe kaa kando lete Munyua Waiyaki, haya ya nne ni kuhusu elimu. Hii mambo ya elimu tuambiwa ni ya bure sio ya bure. Kilasiku unaona watoto wanakimbia hapa njiani. Na hii imevutiwa na wengine kuhusu hii kusema at office maintainance, haya trophy whatever, kwa hivyo tunaona hii constitution munayo itengeneza sasa iyanziwe muelekeo kuwe munaweka kitu ikitoka kule juu, iwe ni hiyo, hiyo, hakuna ingine hapa kando.

Eeh ile ingine ni kuhusu hii pombe haramu; tunasikia kuna pombe haramu hii, na inakataliwa na serikali na inaendelea kua watu hapa. Tunaonelea kama kitu inasemekana ni mbaya, hapana kusikiza hata ikiwa ni mkubwa, na mimi ninanyimwa kwasababu sina uwezo na were mkubwa unapewa na unakuja ku-uwa watu hapa. Kwa hivyo tunaonelea kama sheria inatungwa, inatungwa ya watu wote, sio ya wakubwa na wadogo.

Ile ingine ilikuwa unaona mukiwa pahali mtu anasemekana msheshimiwa ametokea. Msheshimiwa ndio tu mumemchagua na atupatie heshima, na sasa naye msheshimiwa anafaa kupatia heshima kuna wengine wana wakiwa kama ni msheshimiwa akienda pahali ana watu wanamchukuwa kama msheshimiwa lakini yeye haichukuwi kama msheshimiwa kwa hivyo tunaona, tunaonelea hao wawe kiwango moja mtu apewe ile heshima yake na hao wananchi apewe heshima yake. Kwa hivyo yangu ni hayo. Asante sana.

Councilor Musau: Basi kwa Com.issioners eeh, msheshimiwa wetu, members wale wamekuja kutoa maoni ya kubadilisha katiba. Kwanza mimi naomba radhi kwa jana nilijaribu kufika kazi mingi imekuwa, leo nikajaribu kufika kukakuwa na kazi ya kutembea na watoto mpaka karibu mbali mbali kidogo kama kilometre kama kumi. Hivi sasa nimetembea more than about fifteen kilometres na miguu.

Yangu Commissioners nataka muandike, nitalete karatasi baadaye. Commissioners zote zile zimetolewa Kenya hii, kuanzia ile

ya zamani ilikuwa ya Njonjo Commissioner ya kuangalia mchango, Commissioners wa kuangalia mambo ya kila kitu. Sasa mimi katika hii nakalia labala ya nane ya kutengeneza katiba. Na katiba hapana kitu mchezo, katiba ni kitu unatengeneza kesho inakuwa taabu kwako katiba ni kitu unatengeneza kesho inakuwa mzuri kwako kitu ya kwanza mimi nataka kutengeneza pande yangu sababu mimi ni councillor, watu wanasema ile mtu bado soma na bado fike form four hapana chagua. Audience (Laughter) Councilor Msau. Na mimi nasema Rais wa nchi hii x 2 kama anapendwa na wananchi hata kama mezeeka, tuchague huyo kwa sababu ni watu wengi wanapenda yeye, sio katiba ni mwananchi. Na mimi ni chaguliwe hata kama bado soma, sababu ni mwananchi.

Ile ingine nataka sema hapa iko eeh cap.265 ya local government, imeumiza councils zote Kenya. Kwa sababu ikienda katika Nairobi utakuta the clerk of Nairobi ndio boss ya mayor. Na Councillors hawawezi kufanya chochote. Ukija hata mpaka hapa kwetu unakuta councillor analipwa mshahara wa elfu saba. Na saa hii tunasema tutengeneze katiba, elfu saba! Na wewe unasimamia watu ishirini na kitu elfu, sasa kwa nini hii kitu hapana pelekwa huko pale wabunge wanalipiwa, ma councillors nawao waende wakalipiwe hapo.

Audience: Laughter.

Councillor Musau: Ile kitu ingine, uwezo, katika Nairobi pale pako mayor, pale pako mayor ni Nairobi, Machakos, na Mombasa, wapi sehemu hizo. Katiba iangalie wakiongeza mshahara, hapana kuongeza sababu wako Nairobi! Alichaguliwa akaitwa councillor, kabla hajachaguliwa kuitwa mayor, alitwa councillor, kwa hivyo mshahara yake na councillor ya mashambani kama hapa tulipwe pamoja. Sababu the living of the standard imeenda juu, saa hii nikitoka hapa nje nitaanza kuitisha tobacco. Na mshahara attanza kuitishwa ndizi. Wewe ukija kutoa maoni, utaitishwa nini? Haya kwa hivyo sisi tuongezwe mshahara, sababu tuko na kazi mingi. Kitu ingine, katiba hii tunaitengeneza hapana ya katiba hii imeletwa shauri tuu ya watu wana angalia Moi tu! Moi tu! Moi tu! Moi. Leo Moi akitangaza aseme nimetoka kwa kiti hii katiba utasikia wazungu wakisema isimamishwe. Hii katiba, si hao Commissioners wako hapa? Saa hii saa saba Moi aseme mimi mtukufu Rais Daniel Arap nimewacha kazi eeh! Utasikia mzungu akisema eeh katiba ya Kenya simama. Nitafute namna nyingine, Kenya sisi hapana tengeneza katiba ile ya haki, tupewe nafasi hii maoni wewe umekuja hapa leo hapana tunataka ikuje tena.

Maoni ipeanwe kabisa, ipeanwe na yule mtu ambaye yuko kiziwi, kiwete nani! Apeane maoni ya katiba. Kwa sababu sisi tunapelekwa tu kuingizwa kwa msituni. Tunapelekwa tu tuingizwa kwa taabu, tunapelekwa tu tuingizwa kwa miti juu, hatujainizwa kwa mto ndani saa ile tunaletwa na maji mzungu hapana iko! Mzungu atakuwa America, mzungu atakuwa London na watu wa Kenya tunapata taabu hapa. Katiba yetu tuachiwe tutengeneze tukiwa na umaskini au tukiwa na pesa. Tusipelekwe mbio, halafu katiba hii mukishachunguza nyingi mkichukuwa maoni, mupeleke bungeni hata kakaliwe chini sasa sababu hapo ndio panatengezwa act! Hii nyingi mnachukuwa iko Pal Yash Ghai, iko ufungamano Mutava, iko Raila, na ya Raila ni ya bungeni ya Mutava wale wamekuja hapa ambao wana hakilisha Mutava ni ngapi? Hakuna! Wale wamekuja hapa na wanahakikisha ya Pal yash Ghai in hawa! Na sis tumekuja hapa kuwakilisha mjumbe yuko hapa na laini yetu ya Raila.

kwa hivyo katiba hii mpaka ikae iangaliwe sawasawa. Iendelee na isongee, mpaka siku ile katiba ya Kenya itapelekwa bungeni isemwe ndio hii na hii na hii na hii. Ndio sasa tutakubali hiyo ni katiba. Na ikiandikwa, ikikubaliwa tuletewe kwanza tuseme, hii tumekubi, hii tumekataa, hii tumekubali hii tumekataa, sisi wananchi, kwa sababu nyingi mumeleta kwa sisi na mumechukuwa maoni kwa sisi. Mukipeleka huko mturundishe tena, tuje kusema sisi bado zungumza hii tulizungumuza hii lakini muafrika, saa hii anazungumuza saa hii na kesho anasema sio mimi nilikuwa na sema namna hiyo kwa hivyo tuangaliye sawasawa katiba, tuangalie vile tunapeleka huko. Wajumbe, nimesikia watu wanasema wajumbe wanataka wale wako na degree ndio, si umeona wale wako na degree siumesikia hii moja hapa, eeh si-imekuonyesha mtu amechukua shamba tangu 19 siji ngapi mpaka elfu mbili 2930, wewe hutakuwako hata mimi, hata wale wenye kutengeza katiba, tutakuwa tunatengeneza katiba ingine na huyo mtu yuko hapa na nyinyi munaona.

Namunatuambia tutengeneze katiba, kuanza tutaondoa moyo, colony protection tuondowe hawa halafu tutengeneze katiba yetu ya Kenya sababu yeye bado iko na kaa tuu, ni shamba yake na anaka na ile ya zamani, ataendelea na kukana ile ya colony na ile yetu ya langas ilienda kutengeneza ikamwabiya endeleo nakuka. Kwa hivyo commissioners, sisi tunataka muendeleo kuchukua maoni, maoni ya katiba ya Kenya baado. Maoni ya Kenya ya Katiba baado, saa hi utapewa hapa na watu karibu mia mbili, mia mbili, mia mbili, mtu akisimama unaona tuu Moi. Mtu akisimama anaona councillor, mtu akisimama anaona mjumbe siache kitishwe tuu, tutakutana, eeh, kwa sababu wakati ule intakua nikitumiya katiba ile yangu, ile yakuitisha kiti ile yangu na wewe unatengeneza ile katiba ya Kenya, kwa hivyo ni mambo mbili mwenye kuitisha na mwenye kutengeneza.

Kwa hivyo wakati mtu anatoa maoni anatoa ile yake, na hapana guza huko juu (kicheko) sababu huwezifika kwa Mungu kabla pitao kwa Yesu. Tuangalie hapa chini, tutengeneze vile mheshimiwa ameseme, tumeyangawanya mashamba, na Wazungu, Mzungu anaka hapa, na huko kwao London, hakuna Mwafrika. Wanataka kuzungumza, nitawaachia hapo wazungumze ile yangu watoe. Eeh, nitawaacha hapa. Kwa hivyo, sasa tunasema hivi, nyinyi kama mnaona hii Katiba tunasukumwa na Mzungu, museme mbunge ivunjwe, tuitishe kiti. Kama mnaona hii Katiba mtatengeneza i-come sawasawa, muendeleo na kutengeneza, muendeleo na kukaa, hata kama ni 2003 December, mpeane ile haki, hapana neno. Kwa sababu hii Katiba iko mtu anaumwa hapa, anasema “paa” na hapa siku ile tutapelekwa njela hapana pelekwa na yeye.

Com. Kabira: Peana mawaidha.

Cllr. Musau: Ni sawasawa, haya, ile ingine ni kitambulisho, wengi tunatoa maoni, tunasema mtu wa kitambulisho, akisaliwa, kama mama amezaa mtoto na baba, tumezaa mtoto, kitambulisho yake awache kuangaishwa nayo. Kitambulisho yake apewe na ile inaitwa, birth certificate, ni bibi tu, na mama tu au baba atapeleka picha, na kitambulisho anarundi nayo nyumbani siku hiyo. Hii ya kukaa, inaka miaka mingi, birth certificate tu, mtoto amechukua picha, na kitambulisho yake.

Shule, siji tutasema nini. Shule, iko act hawa wanafuata, lakini ile act ya shule, ni kama imeachwa. Siku hizi shule inaenda kama

vile mtu anafikiria. Iko pesa, office maintenance, iko pesa, sijui nini, iko pesa sijui nini, mpaka njioni. Mtoto anakwenda nyumbani asubuhi na jioni. Tengenezeni Katiba, mtoto kama iko miaka ya kuenda nursery, hapana weza kufukuzwa shule upto 18 years, naye atakuwa amemaliza. Akiingia nursery tu, hapana fukuzwa, ni kukaa huko, na kuendelea, na kusoma, kama hapana iko na pesa, baba hapana iko pesa, serikali ilipe baadaye, serikali ilipe. Mtoto akizaliwa America, analipwa pesa, na wetu Kenya, tunataka wakizaliwa na sisi tunaanza kuhesabiwa wetu pesa. Sababu pesa iko, mtoto wangu anahesabiwa pesa kutoka leo nimezaa, mpaka siku ile Mungu atachukua yeye.

Pesa ya wazee, wazee wale wako hapa, wamepata taabu. Iko wazee tunawaita Headmen, na hawa ma-headmen, ndio wako pale chini, huko watu wamegombana usiku kwa kijiji, ni headmen, headman anapeleka kwa assistant chief, assistant chief anapeleka kwa chief, inaenda namna hiyo. Headman muangalie, pahali councillor atalipiwa, na mjumbe atalipiwa, naye headman alipiwe hapo, sababu yeye ana kazi mingi. Na kama hapanalipwa, muangalie tu, itatoka kwenu, na hata nyinyi hakuna account, sijui itatoka wapi, maangalie mtatoka wapi. Maangaliwe, hata kama watapewa kama pension, wewe wakipewa namna hiyo pension, namna hiyo.

Sasa tutaondoka, na tutangojea siku ingine maoni hapa, na hapa tumezikizwa, na iko kitu inatuzikiza pale na iko ingine hapa, (kicheko), na imekamata sauti yangu na imekamata yako. Kwa hivyo, wakati ambayo mtarudisha tena mtuletee, nije nijisikize kama ni mimi nilizungumza hivyo (kicheko) au ni nani, nikumbalie hapo. Kwa hivyo mimi nitafika hapo (kicheko)

Com. Kabira: Asante sana Councillor Musau, Musi Kisuna.

Kisuna: Asante sana, nawasalimu nyote hamjambo.

Audience: Hatujambo.

Kisuna: Maoni yangu ni kidogo tu. Ile ningependa kuongea sana ni upande wa mashule. Upande wa shule, sisi kama wazazi tumeumizwa sana, sana, kwa sababu ni kila wakati kwa wiki, mtoto anawezasoma siku moja. Kwa sababu ni kila asubuhi, mtoto akiamka akienda shule, ikifika saa mbili, mtoto amerundi, leta pesa, na hatujui hizi pesa zinaendaga wapi, ni pesa ambayo hazina receipt. Mwalimu akijaribu kuulizwa na mzazi, hizi pesa, zinaingia namna gani hakuna receipt, nataka receipt, anaambiwa hizi zinaingia mradi mwingine. Na hiyo mrandi hatujui ni mrandi gani.

Ya pili ni upande wa ma-MPs na councillors. Uchaguzi: uchaguzi wa MP na councillor uwe tofauti, wawe na siku yao ya kuchaguliwa.

Ule mwingine, ni upande wa rais. Tukishaachagua ma-MPs na councillors, uchaguzi wa Rais uwe wa baadaye. Na Rais ule atachaguliwa, sio lazima pesa, anatoa pesa na picha yake. Kwa sababu ikiwa ni kutoa pesa na picha yake, kipindi ikiisha,

akikuja huyu, akitolewa, kukikuja president mwingine, naye anatoa pesa na picha yake. Hio sio mzuri. Nataka picha ya pesa iwe tu moja, kama itabeba miaka mia moja iendele, kama dollar.

Upande ule mwingine ni, sub-chief na assistant chief. Chief na assistant chief, hawa ni watu wanaweza kuchaguliwa na raia. Diposa, wawe wanatumikia raia vizuri, kwa sababu chief ako na mamlaka ingine ambayo amejipatia mwenyewe. Na chief anaweza kupewa transfer, awe akikaa mahali kwa muda, anatolewa hapo, anapelekwa kwa muda, hivyo tu.

Ile ingine ni upande wa, huku kwetu sana, Wakamba tunajua kutumia kitu inaitwa kiapo “Kithitu”. Ma-chief wanajua kunyanyasa watu, wengine wale wako na pesa, anaabiwa huyu ni maskini na pengine wanapatana, anataka kunyanganywa kashamba yake, na ni lazima mkamba afuate “kithitu”, hiyo ni lazima iwe iko, muandike hio. Tunajua kutafuta mchanga na njia nyingi.

Ile ingine, upiganji ya kura. Upigaji wa kura, ni lazima kula zote mahali zimepigwa, zihesabiwa hapo. Sio kura, watu wakipiga zinachukuliwa, zinaenda kuhesabiwa mahali hakujulikani. Kula sihesabiwa mahali zimepigwa, na wale watu waliokuwa wanasimamia kula, kama ma-MP’s ni watatu, tunajua mu-MP alikuwa na kura fulani, huyu mwingine mia moja, huyu mwingine mia mbili, huyu mwingine mia tatu. Hiyo mahesabu ipelekwe huko iende ikaongezaniwe huko, tujue ni nani ameshida, katika ma-MP’s na ma-councillors. Ni hayo tu, sina mengi ya kusema.

Com. Kabira: Ahsante sana bwana Kisuna. John Kakui Mutsembi?

Interjection: Ametoka.

Com. Kabira: Ametoka! Justine Kiseli? Mbona leo hakuna mama amekuja hapa kutoa maoni?

Watu wa Kasikeu, hakuna wanawake hapa? Benjamin Mutungi?

Interjection: (Not clear)

Com. Kabira: Benjamin Mutungi? Sorry, Mr. Ole Sutui? That is the D.O.

Interjection: (Not clear)

Com. Kabira: Kennedy Ndambuki?

Interjection: Ameshatoa.

Com. Kabira: Amepeana? Jacob Mwina?

Interjection: (Not clear)

Jacob: Our electoral Commission, wananchi kwa jumla, hamjambo?

Audience: Hatujambo.

Jacob: Yangu ni kidogo, machache.

Interjection: (Not clear)

Jacob: Yangu ni mawili ama matatu. Ya kwanza ni kuhusu electoral Com.ission. Ningependelea zaidi electoral Com.ission iwe independent body sio ati nashindana na mtu na yule nashindana na yeye yeye ameandika yule anahesabu. Hiyo iwekwe kando. Ile inengine limeguzwa kidogo na M.P. wa Kilome, ni judiciary. Hiyo iwekwe kando na Rais. Hiyo ni kama kupunguza uwezo wa Rais kidogo. Judiciary, Rais asitupe mkono ndani, ikae kando na yeye. Ile ya tatu ni wafungwa ama si wafungwa ni washitakiwa. Ni kama wanumia. Tuseme nimeshikwa saa hii, na napelekwa kwa chief camp, nakaa siku moja. Siku tatu huko kwa polisi, nakaa siku tatu bado nangojea tu. Napelekwa kortini (not clear) ikipika siku mbili, nawekwa rumande tena. Siku kumi na nne nangojeahuko na siku ya mwisho inagunduliwa sina kosa. Sasa, hiyo maneno ya 'sina kosa na ninaambiwa niende nyumbani na nimeumia kwa siku nyingi, nitalipwa na nani? Mwandike (laughter). Hiyo iangaliwe, naona ni kama mbaya, na sina mengi, yangu ni hayo.

Com. Kabira: Ahsante sana Bwana Jacob. T. Kimwili? Hayuko? D. Kilonzo of N.C.K.? D. Kilonzo? J. Kiongo? T. Mwema? Munguti Mundo?

Munguti: Ahsante sana kwa nafasi hili nililopewa. Yangu ni maneno mawili tu, si mengi.

Com. Kabira: Mzee songea hivi kidogo watu wakuone. (Not clear)

Munguti: Ahsante sana. Sasa maneno yangu ni hii. Nina (giggles) Mimi ninasikitika sana kabisa sababu toka mimi, mwaka ya 52 hivi, nilikuwa hapa duniani (giggles) na basi tulikuwa tunaitisha ile uhuru. Lakini mimi nafikiri hii location ya sisi hii ya kukaa, sisi hatupati uhuru. Hatuna uhuru. (giggles) sababu yake, kule kikuyuni wakati tulipata uhuru, Kenyatta alinyang'anya wazungu wote ile mashamba yao akawapa watu wao. Lakini sisi hii kwetu hapa ni Ukambani, kutoka. Nairobi mpaka sijui huko karibu kikuyu, wazungu wanapewa hapa, kule wanatoka kama Ndolo, wanapewa shamba hapa, akina Msomba, akina Muyuu hawa wakona mashamba makubwa kabisa na sisi tulikuwa tunapigania turudishiwe hiyo mashamba. Sasa mimi nauliza, tulipata kweli

uhuru tukapewa mashamba yetu? Hapana, sasa hii tunangoja tupate nini ingine kama Moi hivi, tujue kama tunarudishiwa mashamba kidogo na ningependa kama hawa wange gawiwa mashamba. Lakini hapa kwetu, ndio palionekana mahali yakuweka wale watu ile tusha shida kwa vita? Sababu hawa walikuwa wakubwa kwa nini kwa kupigana.

Hapa kwetu ndio iko namna hiyo? Toka Nairobi mpaka Voi. Ukiona hapa, iko mahali ya wazungu, na wazungu wakishaondoka huko, wanakuja Wafrika wengine na Waafrika ndio wabaya kushinda wazungu kwa sababu tulikiwa tunachunga huko kwao. Tunachunga ng'ombe zetu lakini hao watu wetu hii watu weusi, hatuwezi kupeleka ng'ombe yetu huko.

Lakini ningependa hawa, hii mashamba wagawiwe kidogo kwa sababu hawataki kunyang'anywa yote na ile nyengine tupewe. Tukatafutiwe kama acre kumi hivi, tukatakatiwe. Mimi nasema hata ukiondoka hapa uende hapa siku gani hivi uende hivi, utaona mashamba makubwa. Si ndio mimi nasema, sisi bado kupata uhuru. Bado kupata, uhuru sababu mashamba hii tulikuwa tunapigania huko tupate hizo mashamba. Tunangoja katiba hii iwe kama tunaweza kurudishiwa kidogo mashamba. Hata ikiwa wewe huwe umepewa acre 10 hivi ulime, hapana mbaya. Hapo mimi nasema ya pahali ya mashamba.

Ile ingine ya pili ni hongo. Hongo ndio ina zidi sana katika kazi hii ya watu, kama mtu anaingia ndani ya kazi kidogo kubwa anakuwa yeye yuko mbele ya watu au walimu wowote au hata nani. Hongo ni nyingi kabisa. Hata machief, wanataka hongo tu! Kwa nini hawatosheki na ile mahahara wao wanapewa? Hawezi, kutosheka na hiyo. Wanataka hongo tu! Kwa hivyo hongo iishe katika dunia hii. Sijui kama itakwisha. Itakwisha kweli? (Laughter) Hong o? Sijui kama itakwisha lakini iishe. Kwa hivyo, yangu ni hiyo tu kutoka nilikuwa naandika kama hiyo tu. Hongo na kutoka Nairobi mpaka Voi, mashamba, sisi bado, kupata mashamba. Kenyatta yeye kwisha rudishia watu yake huko, ukiona huku ukitoka Kiambu, ukiona huko utashangaa sana sababu vile wazungu walikuwa wanakaa kwa ile kahawa. Hao Waafrika ndio wanaongoza huko, lakini hapa sisi wapi. Hii nchi yetu ndio inapewa hiyo watu kweli? Ambao wanashinda kwa vita ile captain walikuwa wanashinda kwa vita ndio wanapewa. Hii nchi yetu ndio wanape hawa watu kweli? Sisi bado pata uhuru uhuru.

Com. Kabira: Ahsante Mzee, lakini ujiandikishe jina lako tafadhali. (not clear) what is his name? (Not clear).

Thing: I'm Thingi and I'm giving these proposals for the new constitution. One. That we should have free and compulsory education for all children as a mean of poverty eradication. The second: Government Ministries should be abolished and replaced with government departments headed by professionals and experts in the relevant fields as a means of promoting sound governance and professionalism. Third: The powers of the president should be extremely trimmed as a means of separating powers because if he had the three branches of the government, obviously we cannot, have justice in our country.

Fourth: The Parliament should have power to impeach the bearer of the office of the president, incase he commits economic, ills social and political crimes. The fourth proposal is that. All bearers of constitutional offices should be vetted by the Parliament, to ensure that only the qualified hold these offices. The fifth one is that. The constitution should devisely protect the natural resources in particular the taxes paid by the citizens. Seventh: The constitution should provide for tough penalty for

corruption crimes individual who ground institution should not be transferred but instead should be sucked and sued in courts of law. The last one is that. The idle land that we have in our country owned by individuals should be confiscated and given to those who are ready to develop the land. Thank you.

Com. Kabira: Thank you very much Thingi. Do we have Musila.

Musila: Ahsante sana kwa nafasi lakini naomba niruhusiwe kutumia the white man's language. I'll be very brief. The kind of government we have currently, with the President at the top and the Vice-President, to me isn't good system. The only problem is the the powers of the President are excessive and need to be trimmed, so that the separation of powers be seen to be in force so that we have the judiciary, the executive and the Parliament seen to be acting separately. I would suggest that, we would have provision for impeaching the president for abuse of office whether in matters of economic ills , social ills or otherwise.

I would also suggest that there should be provision in the constitution to restrict the number of ministries strictly, maybe not more than 15, and if there is any need to make variations, that should be done by Parliament, at least on a basis of 65% approval. As it is at present, we have too many ministers too many assistant ministers which is gross misuse of public resource. We need few ministries each with one Minister and one Assistant Minister. I would also suggest that all senior appointments be vetted maybe by commissions and the public service be done by public service commission or the Parliamentary commission or any thing else but be vetted by Parliament so as to ensure that people elected or awarded such appointments, have the integrate and competence required so that they are not loyal to the appointing authority. As it is at present, all senior appointments are held on basis of loyalty to the head of state and many of the those appointed to the office is misuse them because they have the protection from the powers that be.

I would also suggest that there should be a code of ethics and conduct, requiring those implicated in scandals to resign forth with pending investigation. I would also suggest that we have an Anti-Corruption Authority, fully entrenched in the constitution and completely delinked from the Attorney General. As we have in Kenya today, the A.G. is quite partisan. I would also suggest that we do not require ordinary offices like that of the auditor and controller general. The auditor and controller general in this country has done wonderful, kind of work but all the reports of the auditor and controller general end up being thrown in the dust bins because his office is toothless.

Reports are tabled in parliament, we read them over the papers and nothings is ever done to these who are implicated by his report. I think there is something technically wrong with that office. We need tenure of office and at least some memo.

We need tenure of office and at least some "memo" for the office of the auditor and controller general, and I think that will work closely with an independent and proper un-corruption authority. I would also suggest that provisions be made during elections

to cater for those out of the country, those in prisons, and those in hospitals. they are still citizens and they have a right to choose leaders in this country. We should not take them as condemned. I would also suggest that the (not clear) distribution of land equitably taking into account the interest of the indigenous people. I would also suggest that the public land corruptly acquired or allocated be possessed and the guilty arraigned in court of law. I would also suggest that we need a unitary constitution as opposed to Majimbo constitution for purpose of enhancing and promoting national unity.

To address un-employment in this country. We need the policy of one man, one job, but qualifications should not be set aside. We should have free and compulsory primary education to create awareness, and address poverty issues effectively. I would also suggest that ministerial appointments although done by the head of state should be pegged to qualifications, and that the parliament be empowered to move a motion censure against any person unfairly appointed to such a position. Thank you

Com. Kabira: Thank you very much Mr. Silas Musila and Peter J. M

Peter J. M.: Thank you very much, for the Com.issioners and fellow electorates. My views are in point forms and I hope that I got to be very brief. I have bout six points to give. One is, since our government has been unable to manufacture more jobs for qualified personnel in this country. I would suggest that one man or one lady be mapped to just one job, and we should shun these habit of being Miss or Mr all knowing in this country, because of these, one person has been holding several jobs or portfolio's for that matter, where as a better qualified person has none.

My second view is that, let us this time around unlike in the past be very strict on job professionalism in this country. One should only qualify for a job for which they have studied at a certain level of study to ensure proper, effectiveness and efficiency at all our work places.

The third view. I am requesting the government to make arrangements to educate, all the rural dwellers on modern information technology, it is very important.

Point number 4, and this one is in Kiswahili. I am requesting the government to institute an act of parliament which take care of "Migogoro ya uridhi baina ya wavulana na wasichana. Sheria iwekwe iwe kwamba wote wanapata pato sawa kwani hata usichan ni uwana pia, na huend maisha ya ndoa yamemshinda".

Hoja ya tano pia iko katika Kiswahili. Sijui ni sheria ipi ambayo Rais wa nchi hutumia kuwapatia high ranking retired military men huge tracks of land. Kwa hivyo na sema hivi Rais apokonywe uwezo huo wa kuwapatia hawa ma-officer wa kujeshi huge tracks of land. Kwa mfano tunayo hapa kina Major retired Musomba Muiyo Mulinge to mention a few. Hiyo ardhi inafaa ichukuliwe na kurudishiwa raia wa karibu ambao wanaihitaji zaidi.

Hoja ya sita na ndio ya mwisho. These one is in English. I think there should be an act of parliament, supporting that our currency should not have the face of a human person anymore. My reason for these is that it generates a feeling that all the money is his or hers, or the person ethnic group. For these matter, I suggest there be a picture of our national flag, on our currency. For those views thank you very much.

Com. Kabira: Okay thank you Mr. Mutisya. May I have Cosmus Mutuku.

Cosmus Mutuku hayuko? B. K. Nzioka, Chekindu group, B. K. Nzioka not here? Samuel Mabwavywa. Endelea

Samuel: Kwa Com.issioners na wale ambao wako hapa, nina furahi kupewa hii nafasi ili nionge kidogo juu ya katiba hii amabao tunataka iingie katika nchi hii yetu. Kabla sijataja kitu, naomba usamaha maanake hii si nzuri exercise. Lakini nitataja kitu. Naanzia na free education ili Kenya yetu iwe na wate ambao wanaelewa, kutoka Std. 1 mpaka Std. 8, na form 1 mpaka form 4, nauliza kama inawezekan iyo iwe kata kata ni free education Kenya nzima.

Nitaenda sehemu ya pile ni mbunge. Namna ya kuchagua mjumbe au mbunge. Mbunge, wale amao wanafanya interview maana kuna watu ambao wanazaliwa wakiwa, wanajua kila kitu lakini hawana education kubwa. Hawa form 4 na form 6, wale wafanye interview na yle ambaye atafanikiwa kupita aingie katika election. Maana kuna born (not clear) na akipita aingie uchaguzini. Graduate na B.A., N.A. na doctor kwenda juu, wasiulizwe ni miaka mingapi maana, kutoka Std. 1 kwenda apite graduate aingie kwa ile nyingine, miaka yake inatosha aingie katika uchaguzi bila pingamizi yoyote. Ana education ya kutosha, anafaa kila kitu, na mataabu yote aliyapata kutoka Std. 1 mpaka doctor or bachelor or arts.

Namba nne, habari ya President. Kiti kikubwa, awe na miaka arobaine na tano na kwenda juu, na awe amekoma kwa kila kitu, na achaguliwe kutoka mahali fulani. Na chama kile chake kikimchagua kupewa hicho kiti (not clear) atakuwa president. Retired officers kwa kile department waendeleo kuongezwa mishahara yao hata akiwa nhe. Wate wengine wakiongezwa deapartment yake na yeye apewe ‘fraction’ fulani, maan yeye ndiye aliendelea na hiyo kazi kwa miaka mingi sana, afikiye hiyo retirement.

Administration: Nitatoka hapa chini tu, sita kwenda kwa mkoa au huko juu. Ni hapa kutoka kwa chief, assistant chief na sub-headmen. Wapewe pesa ya kutosha, maana wakikosa kufanywa hivyo, wanaangamiza wale ambao wanahudumia. Hata wakiambiwa wasifanye chochote, akiwa apatiwi pesa ya kutosha, hiyo mambo itatokea, kwa ma-case, kwa kile njia wanaendelea namna hiyo, na shida ni kupewa mshahara ambao hutoshi. Ya pili, wapewe transfer kama watu wengine. Asikae mahali fulani maana ni kwao, aende mahali pengine x3, na ajue mengi, lakini siyo kukaa mahali pamoja. Sub-headmen yule mtu ambaye hapewi kitu chochote, mzee wa kijiji, afikiwi katika katiba hii ambayo tunahitaji nchi. Sana sana maana kazi ile mingi iko kwa mzee wa kijiji, apewe mshahara kama wengine, aende sawa sawa kama wale watu wengine.

Habari ya mashamba, Kuna mashamba ambayo ilitajwa na watu wengi. Wale wakubwa zaidi. Mtu apewe acre elfu mia moja, elfu mia mbili na kadhalika, na kuna watu wengine ambao wanasumbuka hapo karibu wanaweza kupata. Huyu squatter

anaweza kuishi ndani ya katiba hii yetu. Squatter na ni mtu wa Kenya, hiyo inaweza kuisha katakata. Wagawiwe mashamba kana watu wengine. Watu wa Kenya waitikie tumepewa katiba ambayo inakwenda chini ikafikie yule mdogo sana, na inakwenda juu ina mfikia yule yuko juu zaidi. Kwa hivyo nitkoma hapo, maana mimi sisikie sawa sawa. Asanteni.

Com. Kabira: Asante sana mzee Samuel na pole kwa ugonjwa. Julius Mbithi Kimeu hayuko ? Mutie Muteti

Mutie Muteti: Nawashukuru sana nyinyi ambao mlikuwa kukusanya maoni ya wananchi hapa, kuhusu katiba. Mimi ningependelea sana kuchangia msawaada wa uwezo wa Rais. Ningeonelea vizuri sana huo uwezo wake upunguzwe, kiasi kwamba iwe, hasa sana sana kazi yake ni kuangalia mambo ya serikali yanaenda aje, mambo ya kijeshi ama mambo mengine ya upande wa kihela, upande wa budget awe akiachia mamlaka bunge iwe ikifany budget yenyewe bila (not clear). Sehemu nyingine ningependa kuchangia ni upande wa mishahara kwa wafanyi kazi wote wa serikali. Hasa tukichukua mfano wa walimu na wabunge. Tutapata walimu ni watu wamelipwa kiwango ya chini sana na hali ni wafanyi kazi wa serikali kama watu wengine wa serikali. Ambapo utawakuta wabunge wakikaa kule badala ya kutetea watu wote sana sana wanatetea mishahara yao wenyewe, wanaongezwa. Utapata mtu anapata kama laki tatu, Naye mwalimu anapata kama elfu nne, elfu tano. Hiyo nayo iangaliwe sana kwa upande wa haya marekebisho ya katiba. Mfanyi kazi wowote wa serikali awe atleast amelipwa kitu ambayo inaweza kumsaidia na family yake. Mengine tuangalie upande wa maaskari wetu, Police force. Corruption imeingia sana kwa upande wa police force, na either labda hii kwa ajali ya kulipwa vibaya, ama hawana ma-qualifications ya kuwa ma-police ama haop sijajua.

Pia nayo hiyo iangaliwe sana. Upande mwingine ni upande wa mkuu wa sheria, chief adviser wa serikali awe akichaguliwa na wabunge sio president amchague hapana. Sine mengi ni hayo tu.

Com. Kabira: Asante. Nickson Nzioka, Dennis Mandina, Duncan Kamani, Nickson N. Nzioka Ametoka (not clear) So you want to inherit his vacancy fine go ahead.

Nickson Nzioka: Nitasimama upande wangu (not clear) Nickson K. Nzioka. Hiyo ndiyo majina yangu na kwanza kabla kuongea kitu, narudishia nyinyi asante sana kwa ajili ya kufika upande huu. Pia mimi nakaa sana Nairobi. Nilikuwa nikiomba sana vile naweza kukutana na nyinyi tuongee kidogo, kuhusu hii marekebisho ya katiba. N ile kitu mimi ninaomba kama itawezekana ni katiba tuendele na kurekebisha, nitaongea maneno ya N.S.S.F. kama mtu amepatiwa retrenchment awe anapatiwa pesa yake aende kusaidia watu wake, kuliko kungoja ile miaka 55 years, kwa sababu ukiangalia ile miaka wa akina mama kama nyinyi, for example yule bibi yangu nikikufa, na ninawaambia nyinyi ukweli ile kitu mimi nimeona, kupata hiyo pesa wewe mwanamke ni ngumu sana, kwa sababu utaenda hapa kwa N.S.S.F. au hapa kwetu ni Kasikeu. Bibi yangu atoane na mtu hapa mzee kama wewe, waende Nairobi ambiwe tuu achelewechelewe mara ya mwisho mtu akuje amwambie si unaona tumechelewa?

Tutaenda kesho, na unajua kwa vile mimi nimekufa, bibi anaona wewe mzee utamsaidia, na kumbe sio kumsaidia, utamsaidia kwa mambe ingine. Iyendelee namna hiyo na hiyo pesa ipotee na niko na watoto wanatakiwa kusaidiwa hapa nyumbani. Kwa hivyo nilikuwa naomba nyinyi, kwa kweli kam itawezekana mtu akipatiwa retrenchment, ile kitu inaitwa retrenchment siku hizi alipwe pesa yake. Kuliko pesa ikae hapo, kama for example mimi nipatiwe retrenchment, nipatiwe pesa yangu, nitumie na watu wangu. Nikipata kazi mahali pengine hiyo pes itaendelea nitaenda niingie kwa N.S.S.F. na niendelee na kukatwa pesa tena kuliko pesa ikae hapo na sina income ninapata, na hakuna mshahara ninapata .

